# Kanuni za Smithfield za Maadili na Mienendo ya Biashara

Kujitolea Kwetu kwa Kawaida

Smithfield® Good food. Responsibly.®



**Barua kutoka kwa Rais na Mkurugenzi Mtendaji (CEO)** ........................ ukurasa wa 1

**Utangulizi** ........................ ukurasa wa 2

Fanya jambo sahihi ........................ ukurasa wa 2

Kufanya uamuzi wa kimaadili ........................ ukurasa wa 2

Kuripoti Suala na Kuliendeleza ........................ ukurasa wa 3

Viwango vya Tabia vya Usimamizi ........................ ukurasa wa 4

**Wateja Wetu** ........................ ukurasa wa 6

Ubora wa Bidhaa ........................ ukurasa wa 6

Shughuli za Kuaminika za Mauzo ........................ ukurasa wa 6

**Familia Yetu ya Smithfield** ........................ ukurasa wa 7

Afya na Usalama ........................ ukurasa wa 8

Matumizi ya Dawa za Kulevya ........................ ukurasa wa 8

Haki za Kibinadamu ........................ ukurasa wa 8

Utofauti na Ajira Sawa ........................ ukurasa wa 9

Unyanyasaji, Unyanyasaji na Vurugu ya Kingono ........................ ukurasa wa 9

**Utumishi wa Kuwajibika** ........................ ukurasa wa 11

Mazingira ........................ ukurasa wa 11

Utunzaji wa Wanyama ........................ ukurasa wa 13

**Kufanya Biashara kwa Njia Sahihi** ........................ ukurasa wa 14

Mgongano wa Maslahi ........................ ukurasa wa 14

Zawadi na Burudani ........................ ukurasa wa 17

**Wawekezaji Wetu** ........................ ukurasa wa 24

Udanganyifu ........................ ukiurasa wa 24

Biashara ya Ndani ........................ ukurasa wa 24

Mawasiliano na Vyombo vya Habari na watu wa Umma ambao ni wawekezaji ........................ ukurasa wa 25

**Kampuni yetu** ........................ ukurasa wa 26

Rekodi za biashara ........................ ukurasa wa 27

Uchunguzi wa Serikali, Kuitwa mahakamani na Ugunduzi ........................ ukurasa wa 27

Mali ya Kiakili, Siri za Biashara na Habari ya Siri ........................ ukurasa wa 27

Vyombo vya Habari ........................ ukurasa wa 27

Faragha na Ulinzi wa Data ........................ ukurasa wa 28

**Jamii Zetu** ........................ ukurasa wa 29

**Rasilimali** ........................ ukurasa wa 29

**Nenoi la Mwisho** ........................ ukurasa wa 30

Smithfield
Good food. Responsibly.



**Barua kutoka kwa Rais Wetu na Afisa Mtendaji**

**Mpendwa Familia ya Smithfield:**

Tunaishi katika nyakati ambapo jamii inainua haraka mwambaa wa biashara. Kampuni zinatarajiwa kufanya kazi kwa uadilifu mkuu na kuzingatia kifungu cha mahitaji yanayozidi kukua ya biashara na kisheria. Baadhi ya kampuni zinapambana ili kutimiza changamoto hii. Katika Smithfield Foods tumebahatika kuwa na utamaduni thabiti wa kufanya kazi kwa uadilifu na usawa na wa kutii sheria.

Kanuni za Smithfield za Mienendo na Maadili ya Biashara huweka viwango vya kimaadili na kisheria ambavyo tutamia mkuendeleza biashara yetu. Kupitia Kanuni hii yote, tunazungumza kuhusu jukumu lililokushirikiwa la kutimiza viwango vya juu vya kimaadili na kisheria. Ikiwa hautashiriki lengo hilki, basi Smithfield sio mahalipako.

Tumeunda Kanuni hii kwa kuzingatia sheria zinazoelekeza vipengele vya biashara ya Smithfields.

> **Jukumu:** Tunakubali kuwajibika katika kila tufanyalo. Tunazalisha chakula bora kwa njia sahihi kupitia ushughulikiaji unaofaa wa wanyama, utumishi wa mazingira, kuzalisha chakula salama na cha kiwango bora, umuhimu wa jamii za eneo na kuunda mandhari mema, ya kimaadili na yanayotuza ya kazi ya watu wetu.
>
> **Ubora wa Uendeshaji:** Juhudi zetu za kutafuta ubora wa uendeshaji hazina mwisho. Tunatafuta bila kuchoka fursa za kuboresha jinsi tunavyofanya biashara.
>
> **Ubunifu:** Ubunifu ni sehemu ya DNA yetu. Tunatafuta maino mapya katika nyanja zote za biashara, ikujumuisha njia za kufanya kazi kwa busara zaidi, kuwahudumia wateja vyama na kuifanya Smithfield kuwa kampuni bora.

Katika kusoma Kanuni, utaona karibu kwa kila ukurasa **SEMA!** Tunafanya kila tuwezalo ili kufanya kusema kuwa rahisi na tumetoa njia tofauti za mtu yeyote kuwasilisha swali au mashaka. Hata unaweza kuripoti bila kujulikana kwa kutumia Nambari ya Moja kwa moja ya Maadili ya Smithfield kwenye jalada la nyuma la Sheria hii. Ninaahidi kuwa hakuna atakayelipiza kisasi dhidi yako kwa sababu ya kuuliza swali au kuwasilisha mashaka.

Nina uhakika kuwa utajiunga nami katika kuifanya Smithfield kuwa mahali ambapo sote tunaweza kujivunia kufanya kazi.



**Shane Smith**
RAIS NA AFISA MKUU MTENDAJI
SMITHFIELD FOODS INC.

## Fanya jambo sahihi

Hapa Smithfield, tunajitolea kufanya jambo sahihi katika nyanja zote za biashara yetu. Kufanya jambo sahihi inamanisha kutenda katika nia njema kwa wale wanaotutegemea kufanya kazi zetu: wateja wetu, wafanyakazi wenza wetu, wawekezaji wetu na umma. Inamaanisha kamwe kutofanya chochote ambacho tunaweza kuaibiika kuziambia familia zetu kukihusu au kuona kikiwa kimechapishwa katika gazeti letu la mji wa nyumbani. Inaamisha kufanya kazi kwa uadilifu kwa kila mmoja na wale walio nje ya Smithfield.

Hitaji la kufanya jambo sahihi linatumika kwa kila mmoja wetu, pasipo kujali daraja yake. Kitendo cha mfanyakazi yeyote – kiwe kizuri au kibaya – kinaweza kudhihirika kwenye kampuni na kila mfanyakazi wake. Tunawajibika kwa kila mmoja kwa kufanya jambo sahihi. Inaonyesha kujitolea kwa pamoja kwa viwango vya juu vya kimaadili.

Kanuni za Smithfield za Mienendo na Maadili ya biashara hujumuisha lengo linaloshirikiwa. Hufafanua hali ambapo huenda tukahitajika kufanya jambo sahihi. Sheria na mifano iliyo katika Kanuni inaonyesha sheria na kanuni zinazotumika katika biashara yetu. Ni muhimu kwetu kutii barua na sheria na kuwa tutekeleze wajibu wetu kwa kuwa waangalifu kabisa kwa shughuli za biashara za kimaadili.

Kila mfanyakazi anaombwa kutia sahihi kauli kuwa amesoma Kanuni ya Smithfield ya Miendendo na Maadili ya Biashara na kuwa atatenda kwa kuitii Sheria hii kikamilifu. Jukumu letu la kufanya jambo sahihi, hata hivyo, halifiki mwisho kwa kuisoma Kanuni hii. Tunatarajiwa kuishi tukifanya hivyo.

Sasa, zaidi ya hapo awali, watu wa umma huwa waangalifu kwa maneno na matendo yetu. Tunataka kujulikana kama kampuni ambayo inaweza kutegemewa kufanya jambo sahihi kila wakati. Ikiwa una swali kuhusu inavyomaanisha kufanya jambo sahihi katika hali yoyote au ikiwa unafikiri kuwa yeyote wetu anaweza kuwa anakosa katika wajibu wetu wa kuishi kulingana na Sheria hii, una wajibu wa **KUSEMA!** kama ilivyoelezwa kwenye ukurasa huu. Smithfield hujitahidi kuwa mazingira ya kazi ambapo wafanyakazi hujihisi huru na kutiwa moyo **KUSEMA!**, omba usaidizi na uwasilishe mashaka.

## Kufanya uamuzi wa kimaadili

Tunaamini kuwa ni uwekezaji kwetu na kwa kampuni yetu sio tu kutii, lakini pia kuwa wenye maadili. Tunaweza kuzingatia bora wajibu wa Sheria kwa kufanya mambo sio tu kwa sababu ni lazima tufanye hivyo (mwenendo wa kufuata), lakini kwa sababu ni jambo sahihi la kufanya (mwenendo wa kimaadili)

Katika kuliunga mkono lengo hili, zingatia maswali yafuatayo kabla ya kuamua ikiwa utatenda au la:

**Je, hatua hii ni haramu?**

- Je, inakiuka sheria na na kanuni inayotumika?

**Je, hatua hii ni ya kimaadili?**

- Je, ni ambayo sio ya kuaminika?
- Je, inazingatia maadili na sera za Smithfield?
- Je, ingekuwa vibaya kwangu kutenda au kukosa kutenda?

**Je, hatua hii inaweza kuidhuru Smithfield au kuwadhuru wengine?**

- Je, inaiweka kampuni au mimi katika hali mbaya?
- Je, inasababisha mgongano wa kimaslahi?
- Ni salama, isiyo na heshima au ya kutoheshimu?
- Je ningekuwa na hofu ikiwa hii ingejulikana kwa umma?

Isipokuwa iwapo jibu lako kwa maswali yafuatayo ni "hapana", unapaswa kusita, upate ushauri au kubadilisha mawazo. Ikiwa hauko huru na kipengele chochote cha shughuli husika, basi **SEMA!** Usiyapuuze mashaka yako.

## Kuripoti Suala na Kuliendeleza

**SEMA!** ni neno tulitumialo kufafanua haki na jukumu la kila mfanyakazi kuujulisha usimamizi kuhusu tabia yoyote ambayo haitimizi viwango vilivyotolewa katika Sheria hii.

Kila unapofahamu uwezekano wa ukiukaji wa sera au utaratibu wowote wa Smithfield, au wa sheria, amri au kanuni inayoweza kutumika kwenye Smithfield, ni wajibu wako kuripoti mara moja. Ikiwa una shaka, uliza maswali. Kukosa kuripoti mwenendo unaowezekana wa kutotii au usio wa maadili kunaweza kulifanya tatizo kuwa mbaya zaidi, kuruhusu mwenendo usiofaa kuendelea na kuifanya vigumu zaidi kurekebisha uharibifu wowote.

1. Hatua ya kwanza katika kushughulikia mashaka mengi ni kuzungumza na msimamizi wako au na meneja rasilimali watu. Ikiwa hutapokea jibu la kuridhisha au ikiwa hujihisi huru kuwasilisha suala katika njia hii, unapaswa kuendelea na hatua zinazofuata.

2. Piga simu ya Moja kwa Moja ya eneo lako, iliyo kwenye jalada la nyuma la Kanuni hii. Simu za moja kwa moja ni za siri na hata zinaweza kupigwa bila kujitambulisha, ingawa jinsi unavyotoa maelezo mengi kwa mwendeshaji anayejibu maswali mengi, ndivyo tunavyoweza kushughulikia mashaka yako vyem zaidi. Ukiukaji wote ulioripotiwa wa Kanuni hii kupitia simu ya moja kwa moja huchunguzwa.

3. Zungumza na mwanachama wa Idara ya Sheria ya Smithfield au mmoja wa rasilimali za uzingatiaji za Smithfield zilizorejelewa katika Kanuni hii.

Tutaiweka ripoti yoyote utakayotoa kuhusu kosa lililoshukiwa kuwa siri kwa kiwango tunachoruhusiwa kufanya chini ya sheria au vinginevyo tulivyoruhusiwa kufanya kwa kupewa ukweli na hali, Smithfield haitakubali ulipizaji kisasi dhidi ya yeyote kwa kuwasilisha mashaka, kuwasilisha ripoti za nia njema za mienendo mbaya au kutoa habari kama sehemu ya uchunguzi. Masuala yote ya ripoti yatapitiwa na kutathminiwa, huku hatua zinazofaa zikichukuliwa ilim kuchunguza, kuendeleza na kusuluhisha mashaka yoyote yaliyowasilishwa.

Kuripoti suala hakukulindi kutokana na hatua ya kinidhamu ikiwa ulihusika katika mwenendo mbaya, lakini kunaweza kupunguza athari. Tunatarajiwa kuwa wazi na waaminifu katika kuripoti masuala na kushirikiana katika juhudi za kuyachunguza na kuyasukuhisha.

## SEMA!

***Je, "nia njema" humaanisha nini?***

"Nia njema" umaanisha kutenda kwa uaminifu na bila nia mbaya. Unaporipoti mashaka kwa nia njema, unaamini kuwa mwenendo ulitendeka, ulitoa habari ya ukweli na unafanya hivyo bila nia ya kusababisha madhara yasiyofaa kwa Smithfield au watu wengine.

***Je, inamaanisha nini kuwa usiri utalindwa "kwa kiwango tulichoruhusiwa chini ya sheria"?***

Kuulinda usiri wako unaporipoti mambo mabaya yanayoweza kutendeka ni kitu tunachokichukulia kwa makini. Tutafichua tu utambulisho wako itakapohitajika tufanye hivyo, kama vile ikiwa tutalazimishwa na sheria kufichua utambulisho wako.

***Ninafahamu kuwa mmoja wa wafanya kazi wenzangu ametekeleza ukiukaji hatari wa sera ya Smithfield na huenda ikawa amevunja sheria. Nina hofu kuwa kuripoti kutamfanya mfanyakazi mwenzangu kufutwa kazi. Je, ninapaswa kuripoti ninachokifahamu?***

Ndio, lazima uripoti unachojua kuhusu ukiukaji. Ni jambo la kawaida kuwa ripoti yako inaweza kutatiza eneo la kazi na kuwa na matokeo hatari kwa watu wanaohusika. Lakini kuruhusu mwendo mbaya unaowezekana kupita bila kujulikana kunaweza kusababisha madhara zaidi na kuyafanya matokeo ya kifedha, kisifa na kisheria ya utambuzi unaofuata kuwa hatari zaidi. Kutambua na kushughulikia masuala mapema ni jambo lisilo na usumbufu mwingi.

## SEMA!

***Je, ninapaswa kufanya nini ikiwa nina mashaka kuhusu msimamizi wangu?***

A: Ikiwa unamashaka kuhusu msimamizi wako au haujihisi huru kuripoti mashaka kwa msimamizi wako kwa sababu yoyote, unaweza kuzungumza na meneja mwingine au na mwanachama wa Idara ya Kisheria ya Smithfield, au unaweza kutumia Simu ya Moja kwa Moja ya Maadili.

***Ninadhani kuwa mfanyakazi mwenzangu amekiuka Kanuni na huenda hata sheria. Ninataka kufanya jambo sahihi na KUSEMA!, lakini nina hofu kuwa huenda nikaipoteza kazi yangu ikiwa nitafanya hivyo. Je, ninapaswa kufanya nini?***

SEMA! Sera ya Smithfield huzuia ulipizaji kisasi dhidi ya yeyote kwa kuwasilisha mashaka au kuwasilisha ripoti yoyote ya nia njema ya mwenendo mbaya.

***Je, ni vipi ambavyo kampuni inaweza kunilinda kutokana na ulipizaji kisasi?***

Smithfield itachunguza madai yote ya ulipizaji kisasi na itapawaadhibu watu wote binafsi wanaohusika - hadi na kwa kujumuisha kuachishwa kazi.

## Viwango vya Tabia vya Usimamizi

Wale walio sehemu ya uongozi wa shirika, ambao ni wasimamizi au ambao huwasimamia wafanyakazi wengine, wana jukumu la kuishi wakizingatia Kanuni hii. Usimamizi mara kwa mara huwa hatua ya kwanza ya mawasiliano mfanyakazi anapokuja kuwasilisha mashaka. Ni muhimu kuwa kila aliye katika nafasi ya usimamizi asikilize kwa makini na kujibu ipasavyo.

Wale unaowasimamia na kuwaongoza wanaitazama tabia yako. Mfano wako kama kiongozi wa kimaadili kutafanya mengi kuimarisha utamaduni wa Smithfield wa maadili na kutii kuliko chochote kile tunachoweza kukifanya. Pia una wajibu wa kufuatilia kwa karibu uzingatiaji wa Kanuni na wale unaowasimamia na kuhakikisha kuwa wahusika wengine ambao hutangamana na wafanyakazi wetu wanafahamu na kutii sera na taratibu zetu.

Kuna majukumu machache muhimu zaidi kuliko jinsi unavyopokea na kusuluhisha au kuendeleza mashaka ya mfanyakazi. Mfanayakazi anaporipoti mashaka kwako, wajibu wako:

- Kusikiliza na kushughulikia mashaka,,
- Kuyasuluhisha ipasavyo chini ya hali na
- Kuyaendeleza inavyofaa ili kuhakikisha wanapokea uangalifu wa haraka na unaofaa kutoka kwa utendaji kama vile Rasilimali za Binadamu au Idara ya Kisheria ya Smithfield, kutoka kwa wasimamizi wakuu zaidi, au wote.

Usimtume au kuyatuma tu masuala ya mfanyakazi kwa Simu ya moja kwa moja ya Maadili. Chukua jukumu la kuhakikisha kuwa suala hili linadhibitiwa na kuwa watu wanaofaa wanalifahamu.



# Fanya Jambo Sahihi

Ikiwa utaona jambo lolote unaloshuku kuwa halifai au sio la maadili, una wajibu wa **KUSEMA!** Kwa kufanya hivyo, unaweza kutoa habari inayohitajika kurekebisha hali ya kudhuru ambayo ingeweza kutendeka. Ikiwa huna uhakika ikiwa hali inakuhitaji **KUSEMA!** jiulize maswali yafuatayo:

1. Je, hatua hii ni ya kisheria?
2. Je, hatua hii ni isiyo ya kisheria?
3. Je, hatua hii inazingatia Kanuni za Smithfield za Mienendo na Maadili?
4. Je, hatua hii ni ya kisheria na isiyo ya kisheria?
5. Je, ningejihisi huru ikiwa hatua hii ingefanywa kuwa wazi kwa umma?
6. Je, ningependa ifanyike kwangu?
7. Je, hatua hii ingekuchukuliwa kwa njia nzuri na familia, wafanyakazi wenzangu na wanahisa wangu wa Smithfield?

***Ikiwa jibu kwa swali lolote kati ya haya ni "hapana," unapaswa KUSEMA! na uombe usaidizi!***



# Wateja wetu

## Ubora wa Bidhaa

Wateja na watumiaji wetu – ikijumuisha familia zetu wenyewe – zinatutegemea kutoa chakula kilicho salama, bora na kilicho na lebo sahihi. Vituo na bidhaa za Smithfield ziko chini ya sheria na masharti yanayotolewa na Idara ya Kilimo ya Marekani na mawakala sawa katika nchi zingine yanayohusiana na chakula, usalama, ubora na uwekaji lebo. Tunatoa mafundisho kwa wafanyakazi yanayofaa kulingana na eneo na majukumu yao kuhusu mahitaji haya na taratibu tulizotekeleza ili kuhakikisha kuwa tunayatekeleza. Ni muhimu kuwa tuchukulie mafundisho haya kuwa ya muhimu na tutumie kwa uadilifu taratibu hizo.

Wajibu wa usalama na ubora wa chakula ni wetu sote.

Ikiwa unayafahamu matatizo yoyote yanayohusiana na usalama wa chakula au ukiukaji wa taratibu zetu zinazohusiana na usalama, ubora au uwekaji lebo, **SEMA!** Mwambie msimamizi wako mara moja au utumie yoyote ya vifaa vya **SEMA!** zilizofafanuliwa katika Kanuni hii na uyasuluhishe.

## SgughuShughuli za Kuaminika za Mauzo

Smithfield imejitolea sana kwa shughuli za kuaminika na za usawa kwa wateja wetu wote. Hatutajihusisha katika matangazo au shughuli za mauzo za kupotoza au za udanganyifu. Makala yetu ya kutangaza na mauzo yatazingatia sheria zinazotumika. Malalamiko tunayofanya kuhusu bidhaa zetu na zile za washindani wetu lazima yazingatie ukweli mtupu na kunakiliwa. Matangazo ya uongo au ya kupotoza yanaweza kusababisha matatizo hatari ya kisheria na kibiashara kwetu. Kumbuka kuwa tunashindana kwa usawa kwa misingi ya ubora na bei. Ikiwa unamaswali au mashaka kuhusu mauzo yoyote au shughuli za soko za Smithfield au yeyote wa washirika wetu wa biashara au washindani wetu, wasiliana na mwanachama wa Idara ya Sheria ya Smithfield au **USEME!** kwa kutumia rasilimali zilizoorodheshwa katika Kanuni hii.

## SEMA!

***Jiko lililo kwenye mstari wangu wa uchakataji linapaswa kuchoma bidhaa hadi 145˚. Nimegundua sasa hivi kuwa thermostati inasoma 120˚tu. Huenda ikawa thermostati ina tatizo. Je, ninapaswa kufanya nini?***

Muarifu msimamizi wako na ufuate taratibu za kuwasilisha tatizo. Ikiwa huwezi kusuluhisha suala hili ikatika njia hii, **SEMA!** kwa kutumia rasilimali katika Kanuni hii.

***Ninafanya kazi katika mauzo. Meneja wangu anataka tuwaambie wateja kuwa mmoja wa washindani wetu huenda akaiacha biashara hivi karibuni. Kama ninavyofahamu, hana msingi wowote wa kuthibitisha hili. Ni fununu ambayo tunaweza kuwa tunaanzisha. Je, ninapaswa kufanya nini?***

**SEMA!** Ni vibaya kueneza habari ya uongo kuhusu mshindani. Ikiwa hakuna misingi thabiti kuhusu habari hii, hatupaswi kuirudia.

## Fanya Jambo Sahihi

Usalama wa chakula, ubora na lebo inayofaa ni wajibu wetu mkuu zaidi. Ni sehemu ya kifungu cha uaminifu wa kimsingi tulio nao na kila mtumiaji. Ikiwa haushiriki kujitolea kwetu kwa dhati kwa majukumu haya, basi Smithfield sio mahali pako.



## SEMA!

***Mwanakandarasi anashughulikia jukwaa kuu kwenye kituo chetu bila kofia ngumu au kifaa cha usalama. Je, ninapaswa kufanya nini?***


Kila mmoja katika kituo chetu, ikijumuisha wanakandarasi na wageni, anapaswa kuzingatia taratibu zetu za usalama. SEMA! na umjulishe msimamizi wako au utumie rasilimali zilizoorodheshwa katika Kanuni hii.

***Daktari wangu alipendekeza kuwa nitumie dawa ya kununua kwa duka ili kusaidia kupunguza maambukizi ya sinasi. Lebo ina onyo la kutoendesha mashine huku ninapotumia dawa hii. Mimi huendesha foko kazini. Je, ninapaswa kufanya nini?***

Unapaswa kumjulisha msimamizi wako na msimamizi wa eneo lako wa rasilimali watu. Huenda ukapewa kazi zingine huku unapotumia dawa ambayo inaweza kudhoofisha usalama wako huku unapoendesha foko.

## Familia yetu ya Smithfield

Usalama ni lengo kuu na linalojumuisha kulindana. Tunalindana kutokana na madhara ya kimwili kwa kuhakikisha kuwa taratibu za afya na usalama wetu zinazingatiwa. Pia tunalindana kwa kuzuia ubaguzi na unyanyasaji katika eneo la kazi. Hatukubali tabia yoyote inayokiuka viwango hivi.



## Fanya Jambo Sahihi

Hebu sote tufanye wajibu wetu ili kuhakikisha kuwa sote tunaweza kwenda nyumbani kwa familia na marafiki wetukila mwishoni mwa siku ya kazi tukiwa salama jinsi tulivyowasili.

## Afya na Usalama

Tunalenga kuweka viwango katika tasnia yetu vya afya na usalama wa wafanyakazi. Shughuli zetu huwa chini ya sheria na masharti ya afya na usalama na kwa sera zetu wenyewe. Tunatoa mafundisho kuhusu mahitaji haya kwa wafanyakazi kulingana na kazi na maeneo walipo. Ni muhimu kuwa tuyachukulie mafundisho haya kwa makini na tuzitii taratibu zetu za afya, usalama na ulinzi. Taratibu zetu hutumika kwa wafanyakazi na kwa watu wengine katika vituo vyetu.

Wafanyakazi wanaweza kuwasilisha mashaka ya kazini ya afya na usalama kwa mtaalamu wa usalama wa eneo lao au kwa mfanyakazi wa usalama wa shirika. Ikiwa utaona mwenendo unaokiuka taratibu za usalama au ambao huenda ukasababisha hatari, ni muhimu **KUSEMA!** haraka kwa mmoja wa rasilimali hizi au kutumia taratibu zilizoorodheshwa katika sehemu ya **SEMA!** ya Kanuni, ikijumuisha Simu ya Moja kwa moja ya Maadili ya Smithfield.

## Matumizi ya Dawa za Kulevya

Sisi ni mazingira ya kazi yasiyokubali matumizi ya pombe na dawa za kulevya. Wafanyakazi wanaokuja kufanya kazi chini ya ushawishi wa pombe au dawa za kulevya hujihatarisha wenyewe na kuwahatarisha wafanyakazi wengine. Kiwango hiki hutumika kwa wafanyakazi wote huku wakiwa kwenye mali ya Smithfield na popote huku wakiwa wanafanya kazi. Kwa kweli, hatutakubali umiliki, usambazaji, uuzaji au utengenezaji wa dawa haramu huku mtu akiwa kazini au katika mali ya kampuni.

Ikiwa unatatizo la dawa za kulevya au pombe, usaidizi unapatikana kwako; tafadhali rejelea kifurushi chako cha mafao au uwasiliane na meneja wako wa eneo wa rasilimali watu kwa usaidizi na rufaa ya siri. Ikiwa una maswali kuhusu sera hii au ikiwa unafikiri kuwa mfanyakazi mwingine huenda akawa anakiuka viwango vilivyoelezwa hapo juu, **SEMA!**

Ikiwa unanyanyaswa au unaona mfanyakazi mwingine (au mtu yeyote katika vituo vyetu) akinyanyaswa, **SEMA!** Mwambie msimamizi, meneja wa rasilimali watu wa eneo lako au uchukue hatua nyingine iliyoonyeshwa katika sehemu ya **SEMA!**
ya Kanuni hii, ikijumuisha kupiga Simu ya Moja kwa moja ya Maadili ya Smithfield.

## Haki za Kibinadamu

Tunajitolea kwa ulinzi na uboreshaji wa haki za kibinadamu. Kama sehemu ya biashara yetu kwa njia ya kimaadili na uwajibikaji, tunafanya kazi chini ya sera ma taratibu zinazotumika katika shughuli zetu za ulimwenguni kote ambazo:

- Hukuza fursa sawa na utofauti.
- Hulinda afya, usalama na ustawi wa wafanyakazi wetu, jamii na mazingira yetu.
- Huzuia unyanyasaji na vurugu kazini.
- Huizingatia haki za wafanyakazi wetu, ikijumuisha kupitia malipo ya ajira na mafao shindani na kudumisha haki za wafanyakazi wetu za kutangamana kwa njia huru na kujadiliana kwa pamoja ikiwa watachagua kufanya hivyo.
- Hazikubali kabisa unyanyasaji wa haki za kibinadamu, ikijumuisha matumizi ya ajira ya kulazimishwa au ya lazima ya watoto katika shughuli zetu za wanakandarasi wetu. Ikiwa unafahamu kuhusu unyanyasaji wowote wa haki za kibinadamu, ONGEA!

Kwa mawelezo zaidi kuhusu jinsi ya kuzingatia na kuboresha haki za kibinadamu, rejelea Sera yetu ya Haki za Kibinadamu.

## Fanya Jambo Sahihi

- Karibu na uheshimu tofauti kuhusu kabila, jinsia, dini, historia, n.k.
- Heshimu wafanyakazi wengine katika matendo yako.
- Tekeleza wajibu wako katika kuyafanya mazingira yetu kuwa huru kutokana na matumizi ya dawa za kulevya.

**SEMA!**

***Msimamizi wangu anatupigia kelele kila wakati na leo hata alitishia mtu mmoja katika timu yetu. Sidhani yeyote wetu anafikiri kuwa msimamizi wetu hakika angetoa tishio, lakini inanifanya kutojihisi huru. Je, ninapaswa kufanya nini?***

Mazingira ya Shieldfield lazima yawe huru kutokana na unyanyasaji na vurugu, ikijumuisha lugha ya kukandamiza na matumizi ya vitisho vya aina yoyote. Hata ikiwa huamini kuwa tishio hakika litafanyika, bado inaweza kusababisha uwoga na ukandamizaji na bado inasumbua na haifai. Ikiwa lugha ya kutishia inatumika katika eneo lako la kazi, ONGEA! kwa kutmia mojawapo ya rasilimali zilizoorodheshwa katika Kanuni hii.



## Tofauti na Usawa wa Ajira

Smithfield hujitahidi kuvutia, kufundisha na kudumisha kikosi tofauti cha wafanyakazi kinachoonyesha jamii zetu. Tunajitahidi kutekeleza utamaduni wa kampuni ambao unajumuisha,ulio chanya na unaolenga kutenda. Kuwa na kikosi tofauti cha wafanyakazi huturuhusu kunufaika kutokana na mitazamo tofauti huimarisha ushindani wetu ulimwenguni.

Smithfield ni mwajiri wa fursa ya usawa. Hatubagui dhidi ya mfanyakazi yeyote au mtumaji ombi yeyote, kwa sababu ya kabila, rangi, dini, ukoo au asili ya kitaifa, jinsia, mwelekeo wa kijinsia, umri, ulemavu, hali ya ukongwe, au hali nyingine yoyote iliyolindwa na sheria ya shirikisho. Kwa kuongezea, uzingatiaji kwa sheria zinazotumika za ajira, kama vile sheria za uithinishaji wa kazi, ni muhimu ili kudumisha udhabiti na uadilifu wa kikosi chetu cha wafanyakazi.

Ikiwa unahisi kuwa umebaguliwadhidi yako, unaamini kuwa mtu mwingine amekuwa mwathiriwa wa ubaguzi au una swali kuhusu sera ya kutobagua ya Smithfield, **SEMA!** Zungumza na msimaizi wako wa karibu, meneja wa eneo lako wa rasimalimali watu au watu wengine katika usimamizi. Ikiwa hujihisi huru kuzungumza na msimamizi au meneja wako tumia rasilizali zilizoorodheshwa katika sehemu ya **SEMA!** ya Kanuni hii, ikujumuisha Simu ya Moja kwa moja ya Maadili ya Smithfield.

## Unyanyasaji, Unyanyasaji na Vurugu ya Kingono

Wafanyakazi wetu wana haki ya kufanya kazi bila unyanyasaji, ikijumuisha unyanyasaji na vurugu ya kingono kazini. Unyanyasaji ni tabia yoyote ambayo hudunisha, kukandamiza au kuudhi mtu binafsi na Smithfield haitakubali aina yoyote yake. Pia hatutakubali matumizi yoyote au vitisho vya nguvu za kimwili ili kusababisha madhara ya kimwili, kusababisha mtu kuogopa madhara ya kimwili au kukandamisha mtu kwa njia nyingine ile. Ili kudumisha eneo la kazi lisilo na unyanyasaji na vurugu, lazima tujiepushe na yafuatayo:

- Mwenendo usiofaa – uwe wa maneno, kimwili au macho na uwe umetekelezwa na mtu binafsi au kupitia njia zingine (k.m., barua pepe) – unaozingatia kabila la mfanyakazi, rangi, jinsia au utambulisho wa kijinsia, upendeleo wa kijinsia, asili ya kitaifa, dini, umri, ulemavu wa kimwili au kiakili, habari ya kijeni, hali ya ukongwe au sifa zingine zilizolindwa kisheria.
- Michezo ya Kikabila, kiukoo, kidini au kingono.

## SEMA!

***Mfanyakazi mwenzangu ameniomba kunipeleka mahali. Sijihisi huru kufanya hivi. Je, ninapaswa kufanya nini?***

Zungumza na meneja wa rasilimali watu wa eneo lako au utumie rasilimali zingine zilizofafanuliwa katika Kanuni hii. Wanaweza kukusaidia kushughulikia maombi yasiyotakikana kutoka kwa wafanyakazi wenzako.

- Kuonyesha vibango, kadi, kalenda, katuni, grafiti au michoro ya matusi au, inayoudhi
- Ukandamizaji, lugha ya matusi, uchokozi wa kimwili, kupigana, uhasama, kuwakandamiza wengine au vinginevyo tabia ya vurugu, au maoni yanayoshusha hadhi
- Vitisho vya aina yoyote, viwe vya kimwili, kimaneno, visivyo vya kimaneno au vilivyoandikwa
- Mawasiliano, mguso au uzuiaji wa mtu kupita wa kimakusudi usiohitajika, usiofaa unaotishia au unaoudhi
- Unyanyasaji wa kingono au maombi ya mapendeleo ya kingono
- Jicho la husuda, ishara za kingono, kuonyesha vifaa au picha zinazoashiria ngono, kupiga mlunzi au kuongea kwa kupigia mtu kelele, kutoa maoni ya kushusha hadhi au ya kingono, wasifu au michezo na maoni yanayorudiwa yasiyofaa kuhusu maumbile ya mtu ya kimwili.
- Utani wa vitendo au kushika mtu kwa njia ya vurugu ambako kunaweza kusababisha madhara ya kimwili.
- Kitendo kingine chochote ambacho husumbua au kutatiza bila sababu matokeo ya utendakazi wa mfanyakazi.

Hii inatumika kwa wafanyakazi wote wa Smithfield na mtu yeyote mwingine anayefanya biashara na Smithfield. Hutumika kwenye eneo la kazi na katika mipangilio inayohusiana na kazi na shughuli nje ya eneo la kazi.

Ikiwa unanyanyaswa au uone mfanyakazi mwingine (au mtu mwingine yeyote katika kituo chetu) akinyanyaswa, au ikiwa utashuhudia au kufahamu kuhusu vurugu au vitisho vya vurugu, **SEMA!** Mwambie msimamizi, meneja wa rasilimali watu wa eneo lako au uchukue hatua nyingine iliyoonyeshwa katika sehemu ya **SEMA!** ya Kanuni hii, ikijumuisha kupiga simu ya Moja kwa moja ya Maadili ya Smithfield.



## Utumishi wa Kuwajibika

### Fanya Jambo Sahihi

Sote tunapaswa kujitahidi kujumuisha kanuni za utumishi bora wa kimazingira katika maisha yetu ya kila siku. Mameneja wanapaswa kukusanya maoni kutoka kwa timu zao kuhusu njia za ziada za:

- kupunguza matumizi ya maji/matumizi yasiyofaa ya maji,
- Kutumia tena vifaa vilivyotupwa,
- kuboresha ushughulikiaji na utupaji wa taka,
- kupunguza matumizi yasiyofaa,
- kutumia nishati inayofaa zaidi na
- kupunguza ufungashaji.

Smithfield imejitahidi katika utumishi unaowajibika juu ya rasilimali zinazoathiriwa na shughuli zetu. Maono yetu nikuendeleza uboreshaji katika kupunguza athari za kimazingira. Tutazitoa rasilimali zetu zinazohitajika ili kulinda mazingira na kutoa utunzaji unaofaa wa wanyama wanaotumika katika shughuli zetu.

### Mazingira

Tuko chini ya sheria za kimazingira za nchi na maeneo ambapo tunaendeshea shughuli zetu. Sheria hizo huweka matakwa kuhusu maji safi, hewa safi, utupaji wa taka hatari na siyo hatari, usafirishaji wa vifaa hatari, udhibiti wa vifaa vya kemikali na upangaji wa dharura. Lengo letu ni kutii matakwa haya kwa ailimia 100 katika asilimia 100 ya wakati.



Ikiwa unamaswali yoyote kuhusu matakwa ya kimazingira au ikiwa ungependa kuwasilisha mashaka, unapaswa kushauriana na msimamizi wako wa karibu, mratibu wa kimazingira wa kampuni yako, meanachama wa Idara ya Sheria ya Smithfielf au uwasiliane na Simu ya Moja kwa Moja ya Maadili ya Smithfield. Na kwa kweli, unapaswa **KUSEMA!** mara moja ikiwa utafahamu kuhusu uwezekano wowote wa hali hatari au kuhusu ukosefu wowote wa kuzingatia mahitaji ya kimazingira.

Smithfield hutoa mafundisho kwa wafanyakazi kuhusu uzingatifu wa kimazingira unaofaa kulingana na kazi na maeneo yao ya kazi. Ni muhimu kuwa wafanyakazi washiriki pakubwa katika mafundisho haya na watumie walichojifundisha. Hivi hapa ni vidokezo vichache vilivyoshughulikiwa katika mafundisho hayo:

- Wafanyakazi wanapaswa kuripoti mara moja makosa yote na matoleo kama inavyohitajika na sheria na masharti yanayotumiak ya kifaa.
- Marekebisho yanayofaa lazima yatatekelezwe mara moja ili kupunguza athari zozote mbaya za kimazingira.
- Ruhusa na ithini za wakala lazima zipatikane kabla ya ujenzi wa kituo na kuzingatiwa wakati wa utengenezaji, uwekaji, uanzilishaji na shughuli.
- Mahitaji ya kimazingira lazima pia yazingatiwe kuhusiana na mabadiliko yoyote katika shughuli za kituo.
- Ufuatiliaji unaofaa, kuchunguza na kutathmini lazima kuendelezwe na rekodi sahihi zihifadhiwe.



## SEMA!

***Kazini, niligundua baadhi ya aina ya kioevu kinachofanana na mafuta kikitiririka kutoka kwa pipa lililovunjika kwenye mali ya kampuni na kikiingia kwenye bomba. Je, ninapaswa kufanya nini?***

Huenda ikawa ni wewe tu ulishuhudia tukio hili. Unapaswa **KUSEMA!** na uwajulishe mameneja na waratibu wanaofaa kuhusu tatizo hili. Ikiwa hawatachukua hatua mara moja kuchunguza, unapaswa kupiga simu kwa Simu ya Moja kwa moja ya Maadili ya Smithfield au umfahamishe mwanachama wa Idara ya Sheria ya Smithfield.

***Msimamizi wangu aliniambia nitupe kifurushi cha makaratasi katika jalala. Niliona kuwa baadhi yake ilionekana kuwa ithini za zamani na rekodi za kimazingira. Je, ninapaswa kufanya nini?***

Sera ya uhifadhi wa rekodi za kampunihuhitaji kuwa aina nyingi za rekodi za kimazingira zidumishwe kwa muda usiojulikana. **SEMA!** na uzungumze na mratibu wa kimazingira ili kuhakikisha kuwa ni sawa kutupa rekodi hizo.

## SEMA!

***Nilitambua kuwa wanyama wachache kwenye mimea walikuwa wamekatwa na kukwaruzwa baada ya kupelekwa kwenye vizizi. Ninadhani kuwa huenda walijeruhiwa na baadhi ya vifaa vilivyovunjika katika kizizi chao. Je, ninapaswa kufanya nini?***

Huenda ikawa wewe ndiwe mtu wa kwanza wa kushuhudia tatizo hili. Unapaswa **KUSEMA!** na uwafahamishe wasimamizi. Ikiwa hawatachukua hatua, unapaswa kupiga simu kwa Simu ya Moja kwa Moja ya Maadili ya Smithfield au umfahamishe mwanachama wa. Idara ya Sheria ya Smithfield.

***Ninafanya kazi katika shamba linalofugwa nguruwe na niligundua kuwa mfanyakazi mwingine alipata changamoto ya kumfanya nguruwe kuhama kutoka kwa kizizi chake kwenda kwenye kihenge chake. Mtu huyu alikuwa akitumia kikingi kumsukuma ili asoge.***

Mifumo yetu ya usimamizi hubainisha aina ya kifaa ambacho kinaweza kutumika ili kuwahimiza wanyama kusoga kutoka eneo moja hadi ilingine na kusukuma au kumpiga mnyama ni kinyume moja kwa moja cha sheria hizi. Unapaswa **KUSEMA!** na umjulishe meneja wa shamba na daktari wa mifugo ulichokishuhudia. Ikiwa hatachukua hatua, unapaswa kupiga Simu ya Moja kwa Moja ya Kimaadili ya Smithfield au umwambie mwanachama wa Idara ya Sheria ya Smithfield.

## Utunzaji wa wanyama

Smithfield ni kiongozi katika ukuzaji, ushughulikiaji na uchinjaji bora wa utu wa wanyama wote wanaokuzwa kwa ajili ya chakula. Usimamizi wetu wa wanyama uko chini ya sheria na masharti tofauti na pia sera ya Smithfield, ikijumuisha Ustawi mpana wa Wanyama na Sera za Matumizi ya Antibiotiki na Mifumo ya usimamizi. Smithfield hutoa mafundisho kuhusu mahitaji haya kwa wafanyakazi ipasavyo kulingana na kazi walizopewa na maeneo yao.

Wafanyakazi wanapaswa **KUSEMA!** kwa haraka kwa wasimamizi wao wa karibu au mwanachama wa Isara ya Sheria ya Smithfield au kuwasiliana na Namari ya Moja kwa Moja ya Smithfield ikiwa watafahamu ukiukaji wowote wa mahitaji haya, ikijumuisha ushughulikiaji wowote mbaya halisi au unaotuhumiwa wa kiajali au uliokusudiwa wa wanyama.



## Fanya Jambo Sahihi

Ushughulikiaji unaofaa wa wanyama silo tu jambo sahihi la kufanya; pia ni somo muhimu la kimaadili na jukumu la kimaadili wanalotudai wagawaji wetu, wateja, wafanyakazi wenzetu na la muhimu zaidi, wanyama waliopeanwa kwetu na ambao huwa tunawategemea kwa maisha yetu.

# Kufanya Biashara kwa Njia Sahihi

Tunaahidi kufanya biashara kwa uadilifu. Hii inamaanisha kufanya uamuzi wa kibiashara katika njia zinazoifaidi kampuni yetu kwa jumla. Pia inamaanisha kutii sheria katika shughuli zetu zote za kibiashara.

## Mgongano wa Kimaslahi

Ni muhimu kuwa kila uamuzi wa kibiashara tunaoufanya kama wafanyakazi wa Smithfield uzingatie mahitaji ya Smithfield, sio kwa maslahi au uhusiano wa kibinafsi. Mgongano wa kimaslahi huwepo wakati ambapo maslahi ya kibinafsi ya mfanyakazi au mmoja wa marafiki wake wa karibu au mwanafamilia hutatiza maslahi ya Smithfield. Ni muhimu kuwa tujiepushe na hata muonekano wa mgongano wa kimaslahi.

Karibu migongano yote inaweza kuepukwa au kusuluhishwa ikiwa itafichuliwa ifaavyo. Ikiwa utaona kuwa wewe au rafiki wa karibu au mwanafamilia ana mapendeleo ya kibinafsiambayo yanaweza kuwa na mgongano na jukumu lako la kibiashara au ikiwa unadhani kuwa mfanyakazi mwingine anaweza kuwa na mgongano wa kimaslahi, mfahamishe msimamizi wako au utafute mwongozo kutoka kwa mmoja wa rasilimali zingine za **SEMA!** zilizoorodheshwa katika Kanuni hii.



## SEMA!

### *Kutambua Migongano ya Kimaslahi*

Sio wazi kila wakati ikiwa jambo fulani linaweza kuwa mgongano wa li,aslahi. Ikiwa una wasiwasi kuwa unawezakuwa na mgongano wa kimaslahi unaohitaji kufichuliwa, jiulize:

- Je, rafiki wa karibu, mwanafamilia au mimi tunatarajia kufaidika kifedha kutokana na mwamala au fursa ya kibiashara ambayo ina uwezekano wa kuwa na mgongano na Smithfield?
- Kushiriki katika shughuli hii husika kunaweza kutatiza mahitaji ya kazi kwenye Smithfield?
- Je, kuna hatari kuwa huenda nikageuka na kuweka maslahi yangu au ya mtu mwingine mbele ya yale ya Smithfield?
- Je, ninaweza kuendelea kufanya maamuzi mema ya kibiashara ambayo huyaweka maslahi ya Smithfield kwanza?
- Je, inaweza kuonekana kwa watu wengine kama kwamba huenda nikawa na mgongano wa kimaslahi?

# SEMA!

Mgongano wa kimaslahi unaweza kuwa msingi wa mapendeleo ya fedha ya kibinafsi au kwa familia au uhusiano wmingine wa kibinafsi. Baadhi ya migogoro ni ya kawaida na mingine huenda ikawa vigumu kuigundua. Haya hapa ni maeneo machache ambapo mgongano unaweza kutokea:

- Maslahi ya kifedha: Ikiwa wewe au rafiki wa karibu au mwanafamilia ana maslahi ya kifedha katika mhusika yeyote mwingine ambayo yanaweza kuathiriwa na matendo yako kama mfanyakazi wa Smithfield, unapaswa **KUSEMA!** na ufichue maslahi hayo.

- Familia na uhusiano mwingine wa karibu: Ikiwa unamsimamia mwanafamilia, au ikiwa unatangamana na mwanafamilia au rafiki wa karibu ambaye ni mgawaji au mteja, una angalau muonekano wa mgongano wa kimaslahi. Hii inajumuisha ambapo mwanafamilia au rafiki wa karibu anakuwa mfanyakazi wa, au mwekezaji mkuu katika, au mgawaji au mteja unayeendeleza biashara naye kwa niaba ya Smithfield. Ni muhimu kuwa hujiepushe na hali hizi na katika matukio ambapo zimeithinishwausiruhusu uhusiano wako wa kibinafsi kuathiri, au kuonekana kushawishi, uwezo wako wa kutenda kwa maslahi bora ya Smithfield. Unapaswa **KUSEMA!** na ufichue mgongano huu unaowezekana mara unapougundua.

- Fursa za biashara za nje: Katika baadhi ya hali, huenda ikafaa kuchukua ajira, uwekezaji au fursa zingine za kibiashara za kando na kazi yako katika Smithfield bora shughuli ya nje isitatize kazi yako katika Smithfield. Jihadhari, hata hivyo, kuwa kufanyia kazi, kuwekeza katika au kuwa na miingiliano mingine ya nje na mshindani, mgawaji au hata mteja wa Smithfield kunaweza kusababisha mgongano wa kimaslahi. **SEMA!** na ufichue shughuli za nje ili mgongano unaowezekana uzuiwe.

- FUrsa za kishirika: Huwezi kujifaidi kibinafsi kutokana na fursa ya kibiashara au uwekezaji uliyoigundua kwa sababu ya ajira yako kwenye Smithfield, isipokuwa ikiwa una ithini ya mapema ya kufanya hivyo.


Kumbuka kuwa na mgongano tu wa kimaslahi si ukiukaji wa Kanuni, lakini kukosa kufichua na kupata idhini zinazofaa za mgongano ndio ukiukaji. Ikiwa una maswali yoyote kuhusu ikiwa jambo fulani huenda likawa mgongano wa kimaslahi, **SEMA!** Zungumza na msimaizi wako, meneja wa eneo lako wa rasimalimali watu au Idara ya Sheria ya Smithfield.

***Mimi ni meneja wa Utaratibu wa kituo chetu. Ninafahamu kuwa kampuni ya malori ya ndugu yangu inaweza kututolea huduma bora zaidi kuliko tunazozipokea sasa. Hii ingefaidi Smithfield na ndugu yangu. Je, huu ni mgongano?***

Ndio. Una angalau muonekano wa mgongano na huenda ukawa pia ukawa na mgongano wenyewe. Ikiwa kampuni ya ndugu yako inaweza kututolea huduma nzuri zaidi, huenda tukampa biashara yetu. Lakini yeyote anayetazama hali hii ana uwezekano wa kuhitimisha kuwa unamtuza kandarasi kwa misingi ya muingano ya kifamilia.

Njia ya pekee ya kusuluhisha hii ni kufichua hali kwa Idara ya Sheria ya Smithfield na umruhusu mtu asiye na mslahiya kifamilia kufanya uamuzi wa mwisho.






## SEMA!

***Mfanyakazi mwenzangu katika ofisi yangu amekuwa akitoka kazini mapema Ijumaa alasiri ili aende kwenye kazi yake ya pili. Hii haionekani kuwa vyema kwa wengine wetu ambao hulipwa ujira sawa kwa kazi ya wiki nzima. Je, ninapaswa kufanya nini?***

Ajira ya nje imayotatiza kazi ya Smithfield ni mgongano wa kimaslahi. Unapaswa **KUSEMA!**

***Rafiki wa karibu wa familia anaendesha shamba lililo na uhusiano wa kibiashara na Smithfield. Sina mapendeleo ya umiliki ya moja kwa moja katika shamba, hivyo ninachukulia kuwa sina mgongano wenyewe au uwezekano wa mgongano wa kimaslahi. Je, hii ni sahihi?***

Hata katika hali ambapo hauna maslahi ya moja kwa moja katika biashara ambayo ina shughuli za kibiashara na Smithfield, uhusiano wako na biashara hiyo bado unasababisha angalau muonekano wa uwezekano wa mgongano wa kimaslahi. Katika hali kama hizot, unapaswa **KUSEMA!**, fichua uhusiano ili upate idhini. Katika kisa hiki, uwazi ndio uamuzi bora kwako, kwa mwanafamilia na Smithfield.

## Fanya Jambo Sahihi

Tunataka kujulikana kama kampuni ambayo hufanya jambo sahihi kwa sababu sahihi. Mgongano wa kimaslahi unaweza kudhoofisha uadilifu wa biashara. Hata muonekano wa mgongano unaweza kusababisha tuhuma kwa Smithfield na wafanyakazi wetu. Fichua mara moja hali yoyote unayofikiri kuwa inaweza kuonekana kuwa mgongano wa kimaslahi.

## Zawadi na Burudani

Zawadi za wastani za mara kwa mara na burudani inaweza kuleta nia njema na kuanzisha uaminifu katika uhusiano wa kibiashara. Zawadi zilizozidi zu za bei ghali au burudani iliyopita kiasi inaweza kuleta muonekano kuwa uamuzi wa biashara haufanyiki sawa. Sote tuna wajibu wa kuhakikisha kuwa zawadi na burudani zote tunazoweza kupeana au kupokea kuhusiana na kazi yetu kwenye Smithfield zinafaa na zinazingatia sera na sheria za Smithfield.

### Kupeana na Kupokea Zawadi

Iwe tunapeana au kupokea, zawadi na burudani lazima ziwe:

- hazijaombwa
- zipeanwe na zipokewe kwa uwazi ,
- zisiwe za mara kwa mara na zisiwe za dhamani ya juu sana,
- zinahusiana moja kwa moja na nia njema, juhudi za nia njema ili kujenga uhusiano wa mteja au mgawaji,
- zisiwahi kuwa za pesa taslimu au vitu vinavyoweza kubadilishwa kupesa taslimu kwa urahisi (k.m., kadi za zawadi),
- zisiwahi kuhusishwa na kandarasi inayowezekana, zabuni ya kibiashara au fursa nyingine ya kibiashara,
- zisingatie kanuni za biashara na utamaduni wa eneo,
- ziripotiwe kulingana na sera zinazotumika na
- zisiwe na uwezekao wa kusababisha muonekano wa ubaya au upendeleo.

Kwa kuongezea, wafanyakazi wa Smithfield wanapopeana zawadi kwa washiriki wa kibiashara, kwa kawaida zinapaswa kuwa vitu vilivyoithinishwa vilivyo na nembo ya shirika ya Smithfield na kufanywa kupatikana na mauzo ya kampuni/idara ya uuzaji.

### Burudani ya Kibiashara

Chakula cha wastani na kinachofaa na burudani inaweza kukubalika au kutolewa na wafanyakazi wa Smithfield ambapo nia kuu ya chakula na burudani inahusiana na biashara. Katika visa kama hivyo, mfanyakazi, na pia mteja, mgawaji, mwanakandarasi au mshiriki, lazima awepo.

Ikiwa utaoa zawadi, chakula au burudani, lazima uhakikishe kuwa ripoti na rekodi zako za matumizi zinaonyesha kwa usahihi gharama inayohusishwa.

## Fanya Jambo Sahihi

Uwe mpokeaji au mpeanaji, lazima tujiepushe na muonekano mbaya kwa kuzifuata kabisa sera zinazotumika, ikujumuisha zile za kuripoti zawadi na burudani.



## Maafisa wa Serikali

Miingiliano yetu na maafisa wa serikali huhitaji uangalimu maalumu. Kwa hali yoyote wafanyakazi wa Smithfield hawapaswi kutoa zawadi, chakula au burudani kwa afisa yeyote wa serikali bila idhini inayofaa kutoka kwa Idara ya Masuala ya Shirika na Uzingatiaji au kama ilivyoonyeshwa katika kiteno kilicho hapa chini kwa mada "Kuapmbana na Rushwa na Kupambana na Ufisadi" na "Michango na Shughuli za Kisiasa" na katika Sera na Miongozo yetu ya Kupambana na Ufisadi. Sheria maalumu za miingiliano na mawakala ya serikali yanayodhibiti shughuli za Smithfield, iwe katika kiwango cha kitaifa, jimbo/mkoa au eneo. Hasa, hii hujumuisha chakula, wadhibiti wa kilimo, kimazingira na usalama (nchini Marekani, Idara ya Kilimo ya Marekani (USDA), Usimamizi wa Chakula na Dawa (FDA), na Wakala wa Ulinzi wa Mazingira wa Marekani (EPA) na Usimamizi wa Usalama wa Kikazi na Kiafya wa Marekani (OSHA)).

Hakuna mfanyakazi, wakala, mshauri, mtetezi au wawakilishi wengine wa Smithfield au wanaotenda kwa niaba ya Smithfield wanaweza kupeana kitu chochote cha thamana kwa mkaguzi yeyote au afisa yeyote kutoka kwa wakala wowote wa serikali (shirikisho/kitafa, jimbo/kimkoa au kieneo) kwa kutozingatia kipengele chochote cha shughuli za Smithfield. Uzuiaji huu unatumika kwa zawadi za pesa na pia vitu visivyo vya thamana ya pesa, usafiri, makaazi, huduma (k.m., kuosha gari, kuchukua nguo zilizooshwa), burudani (k.m., tiketi za matukio ya michezo) na ukarimu mwingine na mafao au upendeleo mwingine. Kumbuka kuwa hakuna thamani inayoruhusika ya zawadi na huduma kama hizo. Malipo YOTE, zawadi na huduma haziruhusiwi.

Ikiwa unafahamu hali ambapo zawadi au huduma kama hiyo inatolewa au kuombwa na afisa yeyote wa serikali, unapaswa kuripoti suala hili kwa msimamizi wako, kwa Idara ya Sheria ya Smithfield au kwa kutumia moja ya rasilimali zingine za **SEMA!**.

### *Zawadi na Burudani*

Tunapopeana au kupokea zawadi au burudani ya biashara, kuna hatari kuwa mwenendo wetu unaweza kuhusisha au kuzua muonekano wa mhusika mmoja kutumia zawadi au burudani kumshawishi mwingine vibaya. Miongozo ifuatayo inaweza kukusaidia kushughulikia eneo hili.

- Hukubalika kila wakati – yafuatayo hukubalika kila wakati n bila ilani au idhini ya mapema, bora imeripotiwa na kurekodiwa kama inavyohitajika na sera za Smithfield na hauhusishi afisa wa serikali:
    - Kupeana au kupokea vitu vya kimatangazo (k.m., kofia au shati zilizo na nembo ya shirika), chakula kinachohusiana na biashara au zawadi cha kimsimu zinazohusiana na tamaduni za likizo, bora:
        - Ni za thamani ya chini;
        - Zimeunganishwa na madhumuni halali ya biashara;
        - Hazipeanwi mara kwa mara kutoka kwa chanzo sawa kwa mwaka; na
        - Vinginevyo ilivyoruhusiwa na sheria inayotumika.
- Kamwe Haikubaliki – Yafuatayo kamwe hayakubaliki chini ya hali zozote:
    - Kupeana au kupokea zawadi au burudani yoyote:
        - Kama masharti ya kupata na kudumisha biashara au faida yoyote ya biashara;
        - Kama sehemu ya mapendeleo kwa ajili ya kupata kitu;
        - Katika pesa taslimu au kitu sawia; au
        - Isiyo halali, katika hali mbaya au inayoooweza vinginevyo kuwa ya kuaibisha kwako au kwa Smithfield ikiwa itawekwa wazi kwa umma.

- Kupeana zawadi au burudani yoyote kwa:
  - Mfanyaji uamuzi ambaye kuna uamuzi uliosubiriwa kufanywa unaoweza kuiathiri biashara ya Smithfield.; au
  - Kwa afisa yeyote wa serikali bila idhini ya mapema kutoka kwa Idara ya Masuala ya Kishirika na Uzingatiaji.

- Zawadi na burudani zingine zozote huhitaji baadhi ya viwango vya ukaguzi na idhini ili kuamua ikiwa zinaruhusiwa. Tumia uamuzi, uliza maswali na utafute mwongozo kabla ya kupeana au kuzipokea.

### *Kupambana na Rushwa na Kupambana na Ufisadi*

Kama kampuni ya Ulimwengu, Smithfield iko chini ya sheria tofauti za Marekani na zisizo za Marekani ambazo huzuia malipo ya rushwa kwa maafisa wa serikali a wengine ili kupata au kudumisha biashara au faida nyingine yoyote ya ushindani. Sheria hizi zinajumuisha Sheria ya Shughuli za Kiufisadi za Kigeni za Marekani na sheria na masharti mengine sawa ya kupambana na rushwa na ufisadikama vile Sheria ya Rushwa ya Uingereza. Kwa urahisi, sheria hisi huzuia malipo, kuomba, kupeana au kupokea rushwa yoyote au aina nyingine ya malipo yaliyokusudiwa kushawishi kwa njia isiyofaa yeyote ili kuendeleza maslahi yetu ya kibiashara. Sheria hizi huenda zikatumika pasipo kujali ikiwa malipo husika yasiyofaa yalipeanwa au kulipwa moja kwa moja na mfanyakazi wa Smithfield au na mhusika mwingine (k.m., mawakala, washiriki wa ubia, madalali au washauri) wanaotenda kwa niaba ya Smithfield.

Rushwa sio pesa taslimu au vitu vingine vinavyotoshana nafedha. Kitu chochote kilicho na thamani kilichopeanwa ili kushawishi vibaya mpokeaji ni kibaya. Rushwa inaweza kuwa ya aina nyingi:

- Pesa au vitu vinavyoweza kugeuzwa haraka kuwa pesa taslimu kama hisa na dhamana,
- Zawadi na misaada,
- Malipo haramu,
- Kipunguo cha bei kisichofaa au asilimia ya faida iliyozidi,
- Marupurupu yasiyo ya kawaida, yaliyozidi au yaliyofichwa, matumizi au michango ya kisiasa au kihisani na
- Kupeana kitu chochote cha thamani kwa mpokeaji, mwanafamilia wake au marafiki, ikujumuisha kazi na malipo ya matumizi ya elimu.

## SEMA!

***Meneja wa ununuzi wa mmoja wa wateja wetu wageni alinitajia kuwa mshindani wetu alimwalika yeye na familia yake kwa wikendi ya gofu kwenye kilabu cha eneo. Sina uhakika, lakini ninadhani huenda alikuwa akiashiria kuwa ninahitaji kufanya jambo sawa ikiwa ningependa kuendeleza biashara na mteja huyo. Tumekuwa tukitafuta akaunti hii kwa muda mrefu. Je, ninapaswa kufanya nini?***

Kwenye Smithfield tunashindana tu kwa misingi ya ubora, bei na sifa. Hatutawahi "kununua biashara" kwa zawadi au burudani. Zungumza na msimamizi wako na mtafute mkakati wa kushinda sehemu kubwa ya biashara hii kwa kustahili. Kumbuka kuwa ikiwa hatuwezi kushinda kupitia ushindani wa usawa, hatutaki biashara hiyo. Pia kumbuka kuwa huenda ikawa meneja wa ununuzi alikuwa akitujaribu ili kujua ikiwa sisi ni kampuni yenye maadili. Ikiwa una maswali yoyote kuhusu jinsi ya kushughulikia hali hii, unaweza kutumia yoyote ya rasilimali za SEMA! zilizopeanwa kwenye Kanuni hii.

## SEMA!

***Tunatafuta zabuni ya kuuza bidhaa zetu kwenye serikali ya kigeni. Mmoja wa maafisa wa kigeni anasisitiza kuwa tulipe ili azuru kampuni yetu ili aweze kuona udhibiti wetu wa ubora. Pia anataka kuja na familia yake katika safari hii na anataka kukaa kwenye Walt Disney World wakati wa wikendi kabla ya ziara na anatarajia Smithfield kugharamia gharama yote ya safari. Je, kuna tatizo lolote kwa jambo hili?***

Ziara ya afisa kwenye kampuni yetu kuchunguza kuhusu udhibiti wa ubora ina madhumuni halali na huenda Smithfield ikaiunga mkono. Kabla ya kuithinisha matumizi haya, hata hivyo, unapaswa kupata idhini kutoka kwa Idara ya Sheria ya Smithfield kulingana na Sera na Miongozo ya kupambana na Ufisadi. Gharama za usafiri wa familia na safari ya kando ya Disney World sio gharama zinazofaa za kibiashara na huenda zisilipiwe moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja na Smithfield. Zaidi, ukweli kuwa afisa aliomba, hasa katika wakati ambapo tuzo la kibiashara la kampuni linasubiriwa na serikali, ni ishara ya hatari kuwa unahitaji kufichua kwa Idara ya Sheria ya Smithfield ili iweze kutathmini kwa ukamilifu zaidi ikiwa iithinishe ombi na ziara ya kampuni.

Kuwa wazi, Smithfield ina sera ya kutokubali kabisa aina yoyote ya shughuli ya ufisadi. Huenda usiithinishe, kuwezesha, kufadhili, kukubaliana na au vinginevyo kuhusika katika malipo au upokeaji wa rushwa yoyote, malipo yasiyofaa au malipo yoyote mabaya ya aina yoyote, bila kujali wanaohusika. Hii inajumuisha malipo yasiyofaa yanayohusiana tu na wahusika wa kibiashara (rushwa ya kibiashara) na pia malipo yasiyofaa yanayohusiana na maafisa wa serikali (rushwa rasmi) Zaidi, huenda usiruhusu wahusika wa nje wanaotenda kwa niaba ya Smithfield kujihusisha katika mienendo isiokubaliwa, kwa kuwa shughuli zao bado zinaweza kusababisha dhima kwa Smithfield na kwa wafanyakazi wa Smithfield.

Tafadhali kumbuka kuwa hatari zinazohusiana na rushwa na ufisadi hutiliwa mkazo zaidi kila tunapojihusisha na maafisa wa serikali. Hii inajumuisha shughuli na wahusika wanaomilikiwa na serikali, wanaoendeshwa na serikali au wanahusishwa na serikali. Katika hali hizo, lazima tuwe waangalifu zaidi ili kuhakikisha kuwa shughuli zetu za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja na maafisa hao zinafaa na zinazingatia kikamilifu sheria zote zinazotumika. Lazima pia tuwe waangalifu kuhakikisha kuwa wahusika wa nje wanaotuwakilisha katika shughuli hizo wana sifa nzuri na wanatenda kwa njia sawa ya maadili na kutii.

Smithfield hutoa mafundisho kwa wafanyakazi ambao kazi zao zina uwezekano wa kuwaweka katika hali ambapo masuala haya yanaweza kutokea. Hii inajumuisha kuhusu jinsi ya kutambua "ishara za hatari" zinazoashiria uwezekano wa wasiwasi wa rushwa au ufisadi, hasa wakati ambapo huenda kukawa na baadhi ya kuhusika kwa maafisa wa serikali (k.m., kama mhusika kwa muamala au katika jukumu la kutoa leseni, kuithinisha, kudhibiti, kuchunguza au majukumu mengine ya usimamizi).



Pasipo kujali ikiwa umepokea mafundisho hayo, ikiwa utagundua shughuli yoyote isiyo ya kawaida katika muamala au shughuli nyingine ya biashara **SEMA!** Kutokea kwa ishara ya hatari hakumaanishi kuwa lazima kumetokea jambo lisilofaa, lakini ni ashirio kuwa uchunguzi wa karibu unapaswa kufanyika kabla ya kuendelea.

Ikiwa utashuku kuwa rushwa imetolewa au kulipwa na au kwa mfanyakazi mwingine au na mhusika wa nje anayeifanyia kazi Smithfield, au ikiwa una maswali kuhusu jinsi ya kutumia sheria hizi, unapaswa **KUSEMA!** mara moja kw akutumia rasilimalim zilizofafanuliwa katika Kanuni hii. Habari zaidi kuhusu mada hii muhimu imeonyeshwa katika Sera na Miongozo ya Kupambana na Ufisadi ya Smithfield.

### *Kupamabana na Pesa Haramu*

Pesa haramu ni mchakato wa uyapata mapato ya shughuli haramu kuonekana kupatikana kisheria. Smithfield hutenda kwa kuzingatia masharti yote kuhusu kupambana na pesa haramu. Ikiwa utagundua shughuli inayofanana na pesa haramu, **SEMA!** na wasiliane na Simu ya Moja kwa Moja ya Smithfield au utumie rasilimali zilizopeanwa katika sehemu ya **SEMA!** kwenye kanuni hii.

## SEMA!

***Ninajua kuwa msimamizi katika kampuni yetu amekuwa akiwaambia baadhi ya wafanyakazi waoshe gari ya inspekta wa USDA aliye kwenye eneo mara moja kwa wiki. Haichukui zaidi ya dakika chache za muda wa mfanyakazi. Je, hii ni sawa?***

Kutoa huduma yoyote ya nyongeza kama vile kuosha gari ya inspekta wa USDA ni ibaya na ni lazima kukome na kuripotiwe mara moja. Kukosa kufanya hivyo kunaweza kuwa na matokeo mabaya kwa Smithfield na wafanyakazi husika. **SEMA!**



## Fanya Jambo Sahihi

Smithfiels imejitolea asilia 100 kushindana tu kwa misingi ya ubora, bei na sifa. Hatutafuti faida yoyote ya biashara kwa kutoa au kulipa rushwa au zawadi na huduma zingine zisizo za kisheria. Ikiwa hautashiriki kujitolea huku, basi Smithfiels sio mahali pako na unapaswa kutafuta kazi nyingine.

## Michango na Shughuli za Kisiasa

Hakuna pesa, vituo, zawadi, chakula, burudani au huduma za Smithfield zitakazochangwa kwa afisa yeyote wa kisiasa wa Marekani, mgombea, kampeni, chama cha kisiasa au hatua ya kisiasa bila idhini ya mapema ya Idara yetu ya Masuala ya Kishirika na Uzingatiaji.

Smithfield huamini kuwa haifai kuhusika katika masuala ya ndani ya kisiasa nje ya Marekani ipasavyo, Smithfield wala mfanyakazi hapaswi kufanya mchango wowote kwa afisa wowote wa kisiasa asiye wa marakani, mgombea, kampeni, chama cha kisiasa au mtu sawa au shirika kwa niaba ya Smithfield. Tafadhali pia tazama Sera na Miongozo ya Kupambana na Ufisadi ya Smithfield na kitengo kilicho hapo juu kwa mada "Kuambana na Rushwa na Kupamabana na Ufisadi."

Smithfield huwahimiza wafanyakazi wote kutuzitumia haki zao za uraia kwa kupiga kura na kwa vinginevyo kuwaunga mkono wagombea au vyama vya uchaguzi wa kibinafsi wa mfanyakazi. Wafanyakazi ambao huchagua kujihusisha na shughuli kama hiyo ya kisiasa hufanya hivyo kabisa kwa uwezo wao wa kibinafsi na kifaragha kama raia wanaowajibika na sio kwa niaba ya Smithfield. Hakuna mfanyakazi wa Smithfield atakayetumia pesa zozote au rasilimali zingine za Smithfield kuhusiana na shughuli yoyote ya kisiasa ya kibinafsi wala kumfanya mfanyakazi yeyote kupokea malipo au kurejeshewa fedha zozote moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja kwa mujibu wa mchango uliofanywa nao kwa njia yoyote. Shughuli ya kisisasa huenda sitatize utendaji wa mfanyakazi wa kazi yake kwa Smithfield.

Kamati ya Hatua ya Kisiasa ya Smihfield (PAC) huenda ikaomba wafanyakazi wanaostahiki kwa mchango wa kampeni za kisiasa. Michango ya Smithfield PAC ni ya kujitolea kabisa na sio masharti ya ajira au maendeleo.

## Mashindano wa Kujitegemea na Haki

Smithfield itashindana kwa nguvu, kwa kujitegemea, na kwa haki wakati wote. Miongoni mwa mambo mengine,hii inamaanisha kuwa utafanya uamuzi wote wa ushindani—ikijumuisha uamuzi unaohusiana na kuweka bei, kutafuta zabuni, kutafuta na uzalishaji—bila kutegemea washindani. Matokeo ya ukiukaji wa kupambana na kutoaminika, kunakoweza kujumuisha dhima ya uhalifu wa kibinafsi kwa watu wowote binafsi waliohusika katika ukiukaji, na pia matokeo hatari ya Smithfield.

Sera za Smithfield huzuia makubaliano yoyote—yawe rasmi au yasiyo rasmi, au hata "kuelewa kwa wangwana"—na msindani yeyote kuhusu kuzuia kushindana kwa njia yoyote. Zaidi ya hayo, ili kuzuia hata muonekano mbaya, sera zetu huzuia majadiliano yoyote kati ya Smithfield na mshindani yeyote kuhusiana na habari nyeti ya ushindani.

Wafanyakazi wote wanahitajika kufuata miongozo hii kwa miingiliano yoyote na washindani:


- **Usijadili** bei za sasa au za siku zijazo, nukuu za bei au zabuni, sera za bei, mapunguzo, marupurupu, masharti ya mkopo, au sheria au masharti yoyote mengine ya kufanya biashara
- **Usijadili** habari ya bei, faida au viwango vya faida.
- **Usijadili** mipango ya uzalishaji ya sasa au ya siku zijazo.
- **Usijadili** kukataa kujishughulisha na mgawaji au mteja yeyote.
- **Uiwahi** kukubaliana na kipengele chochote cha kuweka bei au pato.
- **Usikubaliane** na aina za bidhaa tutakazopeana (au ambazo hatutapeana) au sheria na masharti ambapo tutapeana bidhaa zetu
- **Usikubaliane** na upeanaji wowote wa mteja au ugawaji wa soko.
- **Usibadilshe** habari ya siri, bila kushauriana kwanza na washauri.
- Washindani **sio** vyanzo vilivyoruhusiwa vya akili ya ushindani.

Ikiwa mshindani ataleta mada mbaya ya mazungumzo na wewe, unapaswa kukomesha mazungumzo mara moja, kisha **USEME!** mara moja kwa kuripoti tukio hili kwa Idara ya Sheria ya Smithfield. Usibaki katika mazungumzo kwa sababu ya kujaribu kuwa mpole.

Ikiwa ni sehemu ya jukumu lako la kawaida la kibiashara kuwa na miingiliano na washindani—kwa mfano, ikiwa utanunua bidhaa kutoka kwa, umuuzie, mshindani, au ikiwa utaingilianana washindani kama sehemu ya shughuli za ushirika au kama mwanachama wa kikundi cha ushauri au kikundi kingine cha habari —ni lazima uizue miingiliano yako na washindani kwa miamala ya kawaida ya kibiashara ambayo ni sehemu ya wajihbu wako. Hupaswi kubadilishana habari nyeti ya ushindani na msindani au kutumia habari za mawasiliano za mshindani wako kama sehemu ya akili ya ushindani.

Sera za Smithfield pia huihitaji kampuni kushindana kwa haki kila wakati. Kushindana kwa haki kunamaanisha, kwa mfano, kushinda sokoni kwa kutoa bidhaa au huduma bora, kuwapa wateja bei, masharti, au sera zinazovutia, kuwa na sifa nzuri zaidi au thamana ya rajamu na kuwekeza ili kuboresha matoleo ya Smithfield. Kwa upande mwingine, mwenendo usio na madhumuni ila kumdhuru mshindani unaweza kuchukuliwa usio wa haki na hauzingatii sera za Smithfield.

Miongozo ya Kupambana na kutoaminika ya Smithfield imewekwa ili kukulinda wewe na Smithfield. Ikiwa huna uhakika kuhusu kufaa kwa majadiliano yoyote au shughuli iliyopendekezwa, unapaswa **KUSEMA!** kwa kuwasiliana na Idara ya Sheria ya Smithfield kabla ya kujihusisha katika majadiliano au kukubali kushiriki katika shughuli hii.



## SEMA!

***Jana, nilikutana na mtu wa mauzo wa mmoja wa washindani wetu. Alisema kuwa alijua kwamba tulikuwa tunazabuni mara kwa mara zabuni sawa. Aliniambie kuwa sote tungefanya vyema na kutimiza wajibu wetu ikiwa tungekubaliana kupinda eneo na kuzabuni zabuni fulani huku nao wakizabuni zingne. Hii ni sawa, sio?***

La. Makubaliano yoyote ya aina hii si halali. Watu wa mauzo kama wewe tu wameingia jela kwa kuingia katika mipangilio sawa. Unapswa kuripoti majadiliano haya mara moja kwa Idara ya Sheria ya Smithfield au kwa kutumia moja ya rasilimali za **KUSEMA!**.

**Mimi ni rafiki wa meneja wa mauzo anayemfanyia kazi msindani. Hafurahishwi na mwajiri wake na anafikiri kuachana na kazi. Amejitolea kunipa habari kuhusu mipango yao ya mauzo ya mwaka ujao, ikujumuisha habari kuhusu mabadiliko ya bei yanayotarajiwa. Je, ninaweza kukubali kwa kuwa sikumuomba kufanya hivyo?**

Hapana. Tunatafuta akili ya ushindani tu kutoka kwa vyanzo vnavyopatikana kwa umma na miingiliano mipana halali ya kibiashara. Kwa kuwa hukuomba habari haimaanishi kuwa ni sawa kukubali au kuitumia. Hii pia ni njia ya udanganyifu au isiyofaa ya kupata habari shindani na inaweza kusababisha dhima kwa rafiki yako, wewe na Smithfield. Unapaswa kuripoti majadiliano haya mara maoja kwa Idara ya Sheria ya Smithfield au utumie moja ya rasilimali za **KUSEMA!**.

# Fanya Jambo Sahihi

Ikiwa unahusika katika mauzo au ununuzi nje ya Marekani, tumia kwa uaminifu mafundisho na rasilimali zingine zilizotolewa kwako. Ni uangalifu wako tu unaoweza kuisaidia Smithfield kuzingatia majukumu yake ya kisheria katika eneo hili.

## Wawekezaji Wetu

Kuweka rekodisa sahihi na za wakati ufaao zinazoonyesha vyema nafasi yetu ya kibiashara na kifedha ni muhimu kwa viwango vyetu vya maadili na biashara. Hatutakubali matendo ambayo huzuia shughuli zetu za kifedha kutoka kwa wawekezaji na washikadau wengine.

Tunachukua wajibu wetu wa kushirikikiwa kuzingatia kwa uzito viwango na kanuni zote muhimu za uhasibu wa kifedha na kuripoti.

### Ulaghai

Ulaghai humaanisha kudanganya mtu ili kujinufaisha. Unaweza kuwa wa aina nyingi:

- Kuingiza katika rekodi za kifedha habari ya uongo au isiyozingatia viwango vya uhasibu.
- Kuwasilisha ripoti za matumizi ambazo "zimefunikwa" au ambazo hazionyeshi madhumuni ya kweli ya matumizi,
- Kughushi cheki au hati zingine
- Kuchukua au kutumia vibaya mali au pesa za kampuni,
- Kuongeza nambari za mauzo iki kuongeza mapato yaliyoripotiwa,
- Kujaza malalamiko ya fidia ya uongo ya mfanyakazi na
- Kuficha fedha zilizopatikana kwa njia haramu kama mapato halali.

Udanganyifu haramu na makosa kimaadili. Unaweza kuwa na matokeo hatari kwa washiriki na wahasiriwa. Ikiwa utashuku kuwa mtu yeyote (ikijumuisha afisa, mfanyakazi, mkandarasi au mgawaji yeyote) anaweza kuwa ametekeza udanganyifu kuhusiana na biashara yetu, **SEMA!** kwa kutumia rasilimali zilizopeanwa katika Kanuni hii.

### Biashara ya Ndani

"Habari ya ndani" ni habari yoyote isiyo ya umma ili ya muhimuvya kutosha kuwa inaweza kuathiri bei ya dhamana ya kampuni ikiwa itafichuliwa. Hii inaweza kujumuisha, kwa mfano, habari kuhusu tuzo la mikataba muhimu, mapato yanayotarajiwa au ununuzi au mauzo ya kitengo cha biashara.

Wafanyakazi hawapaswi kuuza dhamana zozote za kampuni huku wakifahamu habari ya ndani kuhusu kampuni au kupitisha habari hiikwa wengine ambao wanaweza kuitumia kufanya biashara na thamana hizo. Kizuizi hiki hutumika katika kufanya biashara katika deni la umma la Smithfield, na pia katika hisa au thamani zingine za kampunitunazofanya nazo au tunazoweza kufanya biashara nazo ampapo wafanyakazi wanaweza kuwa na habatri ya ndani. Sheria za nchi nyingi, ikujumuisha Marekani, huzuia kufanya biashara huku ukiwa na habari ya ndani.

Adhabu ya ukiukaji wa sheria za biashara ya ndani ni kali na sheria ni changamani. Unapaswa kutafuta usaidizi kutoka kwa Idara ya Sheria ya Smithfield ikiwa unamashaka yoyote kuhusu zinavyotumika.

Isipokuwa kwa idhini ya mapema ya Idara ya Masuala ya Kishirika na Uzingatiaji ya Smithfield, huenda wafanyakazi wasifanye biashara kwa bidhaa yoyote soko za siku zijazo kwa akauntiyao wenyewe (isipokuwa shughuli halali za uondoaji hasara kwa ukulima wa kibinafsi) au kijuhusisha na biashara, uwekezaji au miamala ya kifedha ya aina sawa. Wafanyakazi wanaotamani kujihusisha katika shughuli za uondoaji hasara kwa ukulima wa kibinafsi wanapaswa kupata idhini kutoka kwa wasimamizi wao wa karibu.

## Mawasiliano na Vyombo vya Habari na Watu wa Umma walio Wawekezaji

Tunatambua wajibu wetu wa kutoa habari kamili, isiyochelewa, sahihi na ya lengo kuhusu utenda kazi wetu wa kifedha na kiutendaji, na pia mkakati na matarajio yetu. Sera ya Smithfield ni ya kufanya ufichuzi sahihi na usiochelewa kwa kuzingatia sheria za thamani na kuwasiliana kikamilifu na kwa usahihi na vyombo vya habari na jamii ya wawekezaji.

### Vyombo vya Habari

Ni muhimu kuwa Smithfield izungumze kwa sauti moja. Mawasiliano yote na vyombo vya habari – ikijumuisha vyo vya habari vya jadi na vituo vyawavuti – vinapaswa kuelekezwa kwa Idara ya Masuala ya Kishirika na Uzingatiaji.

### Jamii ya Wawekezaji

Idara ya Masuala ya Kishirika na Uzingatiaji ina wajibu wa kusambaza habari kwa na miingiliano na, wachanganuzi wa kifedha na wawekezaji wa kitaasisi na kibinafsi. Hii inajumuisha habari muhimu kuhusu utendakazi wa kifedha wa kampuni, kama iliyoripotiwa katika matoleo ya habari ya mapato ya mauzo ya kila robo mwaka, faili za udhibiti na ufichuzi mwingine wa umma. Maswali yote yanayohusiana na uwekezaji kutoka kwa wawekezaji wa kitaasisi na wa kibinafsi na wachanganuzi wa kifedha yanapaswa kuelekezwa kwa Idara ya Masuala ya Kishirika na Uzingatiaji ya Smithfield.

## Fanya Jambo Sahihi

Kumbuka mali yetu muhimu, kama watu binafsi na kama kampuni, ni uaminifu wetu. Matendo ya mfanyakazi yanaweza kuonekana kwenye uaminifu wa kampuni yetu na kwa sifa za wafanyakazi wenzetu.

## SEMA!

***Nilimuona mkubwa wangu nje na familia yake kwenye mkahawa mpya mjini usiku wa Jumamosi iliyopita. Jumatatu iliyofuata, mkubwa wangu alinipatia risiti kutoka kwa mkahawa sawa wa usiku wa Jumamosi na akaniambia niwasilishe ripoti ya matumizi ya chakula hiki. Hii haoionekani kuwa sahihi kwangu, lakini ninaogopa kuwa nitaingia katika matatizo ikiwa nitakataa kuweka risiti kwenye ripoti ya matumizi. Je, ninapaswa kufanya nini?***

Unapaswa **KUSEMA!**mara moja Tunaelewa kuwa inachukua ujasiri kuripoti mkubwa wako. Tafadhali fahamu kuwa sera ya kutolipiza kisasi ya Smithfield huwalinda wafanyakazi kutokana na ulipizaji kisasi wa aina yoyote.

***Ninafanya kazi katika Idara ya Uhasibu ya Smithfield Mwanahabari wa sehemu ya biashara wa gazeti aliacha ujumbe kwangu akisema kuwa anataka kuzungumza na mimi ili kupata baadhi ya habari kuhusu fedha za Smithfield. Je, ninapaswa kufanya nini?***

Wasiliana na Idara ya Masuala ya Kishirika na Uzingatiaji ya Smithfield kabla ya kutoa habari kuhusu kampuni kwa mtangazaji yeyote wa nje au mhusika sawa. Unapokuwa na shaka, uliza!



## Kampuni yetu

Kuweka rekodisa sahihi na za wakati ufaao zinazoonyesha vyema nafasi yetu ya kibiashara na kifedha ni muhimu kwa viwango vyetu vya maadili na biashara. Hatutakubali matendo ambayo huzuia shughuli zetu za kifedha kutoka kwa wawekezaji na washikadau wengine. Tunayachukulia kwa uzito majukumu yetu yaliyoshirikiwa ya kuzingata viwango na sheria zote muhimu za uhasibu wa kifedha ba kuripoti.

### Mali Yanayoonekana

Mali ya Smithfield yanayoonekana – mijengo, magari, vifaa na bidhaa zake – ni vifaa ambavyo hutuwezesha kufanya kazi yetu. Tuna jukumu la kuyalinda mali hayo. Ikiwa una fahamu kuhusu uharibifu au matumizi mabaya ya mali, zungumza na msimamizi wako wa karibu mara moja au utumie mojawapo ya rasilimali za **KUSEMA!** zilizoonyeshwa kwenye Kanuni hii.

### Mifumo ya Habari na Mawasiliano

Wafanyakazi upewa ufikiaji wa mifumo ya simu, kompyuta, barua pepe na barua ya sauti na rasilimali zingine za kielektroniki ili kuwasaidia kufanya kazi zao. Rasilimali hizo zimemilikiwa au kukodishwa na kampuni. Wafanyakazi wanatarajiwa kutumia rasilimali hizi kwa njia ya kitaaluma, kimaadili na kisheria na kulingana na sera za Smithfield kuhusu matumizi ya teknolojia.

Smithfield humiliki na kudhibiti ufikiaji wa vifaa vyote vya mawasiliano, ikijumuisha kompyuta, programu, barua pepe, barua ya sauti, vifaa vya mikutano na bidhaa za ofisi. Mawasiliano, data na habari unayoituma au kupokea kwa kutumia mali ya kampuni ni mali ya kampuni na sio mawasiliano ya kibinafsi. Smithfield ina haki ya kufuatilia mawasiliano yote, ikijumuisha matumizi ya intaneti na mfanyakazi hapaswi kuchukulia mawasiliano kama hayo kuwa ya kibinafsi au ya faragha. Kufikia na kusambaza makala za ponografia au yanayokera kwa intaneti, barua pepe au kwa njia nyingine yoyote hakuruhusiwi.

## SEMA!

***Nilipata orodha ya mishahara ya sasa na mapendekezo ya ongezeko la malipo katika idara nyingine kwenye mashine ya kunakili kwenye chumba cha kunakili. Je, ninapaswa kufanya nini?***

Orodha hii ina habari nyeti ya siri, ya umiliki ambayo ni lazima ilindwe. Fanya jambo linalofaa na ulete orodha hii kwa meneja wako wa rasilimali watu wa eneo wa biashara yako. Hupaswi kujadili habari hii na watu wengine ndani au nje ya kampuni.

***Ninatambua kuwa mmoja wa wafanyakazi wenzangu huacha habari nyeti ya uuzaji mara kwa mara kwenye dawati lake anapoenda kula chakula cha mchana. Je, ninapaswa kufanya nini?***

Zungumza na yeye na upendekeze kwa busara kuwa afungie habari hii kila anapototoka kwenye dawati. Ikiwa tabia hii haitabadilika, zungumza na meneja wako.

## Fanya Jambo Sahihi

Sote tunaweza kutekeleza wajibu wetu wa kulinda habari ya siri kwa:

- Kuzizingatia sera za Smithfield za udhibiti wa rekodi na matumizi ya teknolojia.
- Kutoshirki manenosiri.
- Kamwe kutoiacha habari ya siri ambapo inaweza kupatikana.
- Kuzima au kutoka kwenye kompyuta wakati ambapo hazitumiki.

## Rekodi za Biashara

Smithfiels hudumisha rekodi sahijhi na kamili za shughuli za biashara. Pia tuna wajibu wa kulinda usiri wa habari tunayotumia katika biashara yetu. Vitabu za Smithfield, rekodi, taarifa za akaunti na kifedha vi rasilimali muhimu za biashara na zote zinapaswa kudumishwa katika njia inayofaa, huonyesha inavyofaa (kwa wakti unaofaaa) miamala ya kampuni na huzingatia sheria na masharti yanayotumika, Kanuni za Marekani zilizokubaliwa za uhasibu na mfumo wa Smithfield wa udhibiti wa ndani.

Sera ya Smithfield ya Usimamizi wa Rekodi huongoza uhifadhi wa rekodi zote za sasa za biashara na pia utupaji wa rekodi zilizopitwa na wakati. Rekodi za kampuni hujumuisha barua pepe, data, hati au rekodi zinazoundwa, kupokewa au kudumishwa kama sehemu ya shughuli za biashara za Smithfield. Rekodi za kampuni pia huenda zikajumuisha vidokezo vya kibinafsi, kalenda na shajara.

## Uchunguzi wa Serikali, Hati za kuitwa mahakamani na Ugunduzi

Mara kwa mara, Smithfield huenda ikahitajika kutoa hati na habari nyingine kwa mawakala ya serikali au katika kesi za mahakama. Idara ya Sheria ya Smithfield ina wajibu wa kuhakikisha kuwa kampuni inatimiza wajibu wake katika visa hivyo. Wafanyakazi wanaoombwa kushiriki katika kutoa hati wanapaswa kufanya hivyo mara moja na kwa ukamilifu. Ikiwa una maswali yoyote kuhusu masuala haya, unapaswa kuwasiliana na Idara ya Sheria ya Smithfield.

## Mali ya Kiakili, Siri za Biashara na Habari ya Siri

Mali ya Kiakili, Siri za Biashara na Habari ya SiriSmithfield huthamini sana mali yake ya kialiki, siri za biashara na habari ya siri. Pia tunaheshimu haki za mali ya kiakili ya wengine. Mali ya kiakili ambayo wafanyakazi wetu huunda, kupata, kuanzisha, kugundua au kuandikahuku wakiwa wameajiriwa na Smithfield na yanahusiana na biashara ya Smithfield ni mali ya - na yanapaswa kufichuliwa mara moja na kupeanwa kwa - Smithfield. Wafanyakazi wanazuiwa kutumia mali ya kialikili ya Smithfield katika njia yoyote isiyoithinishwa au madhumuni yoyote isipokuwa kwa manufaa ya Smithfield. Zaidi, matumizi yoyote ya mali ya kiakili yanayomilikiwa na wahusika wengine lazima yaithinishwe chini ya leseni au idhini kutoka kwa anayemiliki.

Kwa siri za biashara za Smithfield na habari nyingine ya siri, ni muhimu kuwa wafanyakazi wetu waiweke kuwa siri kabisa na kutoificua au kuitumia nje ya Smithfield bila ulinzi wa makubaliano ya siri. Zaidi, wafanyakazi wanazuiwa kutumia au kuwafanya wengine kutumia siri za biashara na habari ya siri ambayo inamilikiwa na wahusika wengine, kama vile wafanyakazi au washindani wa hapo zamani, bila idhini kutoka kwa wamiliki wa habari hiyo. Lazima pia wafanyakazi wazingatie kabisa masharti ya usiri yanayohusiana na habari iliyopokewa kutoka kwa wahusika wengine chini ya makubaliano ya usiri kama sehemu ya ajira yao na Smithfield.

Wafanyakazi wote wa Smithfield wana jukumu la uaminifu kwa kampuni. Ikiwa kazi yako na Smithfield itatamatika kwa sababu yoyote, lazima urudishe kwa Smithfield mara moja mali yote ya kiakili, habari ya siri, siri za biashara na mali mengine ya Smithfield unayomiliki. Zaidi ya hayo, lazima uendelee kuziweka kuwa siri kabisa siri za Smithfield za biashara na habari nyingine ya siri. Huenda usiitumie kwa madhumuni yoyote, ikijumuisha katika biashara yoyote ya siku zijazo, kazi mpya au madhumuni mengine ya kibiashara au yasiyo ya kibiashara.

## Mitandao ya Kijamii

Mitandao ya kijamii (kama vile, Facebook, Twitter, YouTube) ni vifaa muhimu vya mawasiliano ndani na nje ya kampuni. Majukwaa haya muhimu ya ushirikiano wa kimtandao yanabadilisha jinsi tunavyofanya kazi, yakitoa njia mpya za kuwashirikisha wateja, wafanya kazi wenzetu na ulimwengu kwa jumla. Ikiwa itatumiwa kwa busara, inaweza kusaidia kujenga uhusiano wa bishara ulio thabiti zaidi, na wa ufanisis zaidi.

Kwa kuwa ni muhimu sana, majukwaa haya pia huhusisha hatari fulani na huunda wajibu mpya wa wafanyakazi. Huenda wafanyakazi wa Smithfield wasitumie mitandao ya kijamii kwa madhumuni ya kibiashara isipokuwa iwapo wanazingatia sera ya Mitandao ya Kijamii ya Smithfield na Sera ya Mawasiliano. Ni muhimu ufahamu matokeo yote ya kijuhusisha katika aina za mazungumzo ya mitandao ya kijamii na kimtandao ambayo hurejelea kmpuni yetu, bidhaa zetu na uhusiano wako na kampuni yetu na pia kutambua kuwa kampuni yetu inaweza kuhusishwa na tabia zako. Ikiwa utachagua kutambua Smithfield kama mahali pako pa kufanya kazi au ikiwa utachagua kushiriki au kushirikisha maudhui ya Smithfield, lazima utende kwa njia ya kitaaluma. Maswali kuhusu sera zetu na matumizi ya makala zinazoweza kuwa zinamilikiwa na watu wengine yanapaswa kutumwa kwa Idara ya Sheria ya Smithfield. Ikiwa unafahamu ukiukaji wowote wa Sera yetu ya Mitandao ya Kijamii ay Sera ya Mawasiliano, **SEMA!**

## Faragha na Ulinzi wa Data

Kupitia kazi yetu katika Smithfield, huwa tunafikia mara kwa mara, habari isiyo ya umma kuhusu kampouni na shughuli zake. Sote tuna jukumu la kutoshiriki habari hii na yeyote nje ya Smithfield isipokuwa iwapo tuna idhini inayofaa na ufichuajiunazingatia sera ya kampuni. Hii inajumuisha kulinda habari ya kishirika na kiutendaji, uwekaji bei na habari nyingine ya kifedha, habari kuhusu wagawaji na habari kuhusu wateja.

Katika shughuli ya kawaida ya biashara, pia tunadumissha na kuchakata mara kwa maradata ya kibinafsi ya wafanyakazi wa kampuni na huenda pia tukashughulikia data ya wahusiska wa nje. Ushughulikiaji unaofaa wa data hiyo huongozwa na sheria tofauti katika mamlaka tofauti ambapo tunatenda kazi na tunajitolea kuzingatia kikamilifu sheria hizo. Katika baadhi ya visa, sheria inayotumika huweka viwango vya juu sana vya utunzaji kuhusu njia ambayo ni lazima tushughulikie, kuchakata na kudumisha uadilifu wa data ya kibinafsi. Ili kuhakikisha uzingatiaji wa viwango hivyo, wafanyakazi wote, bila kujali walipo wanapaswa:

- Tazama "data ya kibinafsi" katika maneno mapana sana, kujumuisha habari yoyote ambayo hujumuisha au huhusiana na mtu binafsi anayeweza kutambulika (iwe kwa kurejelea jina, nambari ya utambulisho au kitambulishi kingine).
- Fikia data ya kibinafsi tu ikiwa umeithinishwa na unahitaji kufanya hivyo kwa sababu halali za kibiashara.
- Jihadhari kulinda data yako ya kibinafsi kutokana na kupotea, matumizi mabaya au ufichuzi, ikujumuisha kwa:
    - Kupunguza ukusanyaji na matumizi ya data ya kibinafsi;
    - Kuhakikisha kuwa data ya kibinafsi inadumishwa na kushughulikiwa kwa usahihi na usalama; na
    - Kutoshiriki au kuifanya data yoyote ya kibinafsi kupatikana kwa yeyote bila idhini na sababu halili ya kibiashara ya kuipokea au kuifikia.
- Mjulishe mara moja mwakilishi wa  wa Idara ya Sheria ya Smithfield endapo utafahamu au kuwa na mashaka kuwa huenda kumekuwa na ukiukaji, ambapo uharibifu wa kiajali au haramu, hasara, mabadiliko, ufichuzi usioithinishwa wa ufikiaji usioidhinishwa wa data ya kibinafsi unawezakuwa umetokea.

Sheria hii ya arifa hutumika kwa njia sawa kwa mashaka kuwa ukiukaji unaweza kuwa ulitokea kwa mjibu wa data ya kibinafsi kudumishwa, kusambazwa au kuchakatwa vinginevyo na Smithfield, na pia kwa mujibu wa data ya kibinafsi kudumishwa, ksambazwa au kuchakatwa vinginevyo na mhusika wa nje, kama vile mtoaji huduma anayetenda kwa niaba ya Smithfield.

Ikiwa una mashaka yanayohusiana na faragha au ulinzi wa data, **SEMA!** Mwambie msimamizi wako, mwakilishi wa Idara ya Sheria Smithfield au uchukue hatua iliyoonyeshwa katika sehemu ya **SEMA!** ya Kanuni hii, ikijumuisha kupiga simu ya Moja kwa Moja ya Maadili.

Kwa maelezo zaidi kuhusu jinsi Smithfield hulinda faragha ya data, tafadhali rejelea Sera yetu ya Faragha.

# Jamii Zetu

Tumejitolea kwa ustawi unaoendelea wa jamii zetu ambapo tunafanya kazi. Kuonyesha kujitolea huku, Smithfield hulenga kusaidia elimu na fursa za ukuaji katika miji ya mashambani kote Marekani, ikijumuisha kwa watoto na wajukuu wa wafanyakazi wa Smithfield. Juhudu hizi, hata hivyo, huwakilisha sehemu tu ya juhudi za upeanaji za hisani za Smithfield.

Kampuni na tanzu zake zinajishirikisha na mipangi mingine mingi ya kihisani ikijumuisha kujitolea na matoleo kama vile Kuzilisha Familia zilizo na Njaa, Mpango wa Kulinganisha zawadi wa Wafanyakazi wa Smithfield na Kupeana kwa Jamii ili kusaidia mipango mingine ya eneo. Biashara za Smithfield huhimizwa kurejelea Mwongozo wa Upeanaji wa Kihisani wa Smithfield na kuratibu michango kama hiyo na Idara ya Masuala ya Kishirika na Uzinggatiaji ya Smithfield.

# Rasilimali

Kama tulivyotaja kwenye**ukurasa wa 3**, tunatumia neno **SEMA!** kufafanua haki na wajibu wa kila mfanyakazi kuujulisha usimamizi kuhusu tabia yoyote ambayo haiambatani na viwango vilivyoonyeshwa katika Kanuni hii au kuuliza swali kuhusu viwango hivyo. Kuna njia kadhaa ambavyo unaweza **KUSEMA!**

1. Zungumza na msimamizi wako au na meneja wako wa eneo wa rasilimali watu. Katika visa vingi, hii itakuwa njia rahisi zaidi ya kusuluhisha mashaka yako. Ikiwa hii haitasuluhisha mashaka yako au ikiwa haujihisi huru kuwasilisha suala kwa njia hii, unapaswa kuchua hatua moja au zaidi ya zilizopeanwa hapa chini.

2. Zungumza na mwanachama wa Idara yako ya eneo ya Sheria ya Smithfield.

| | | |
|---|---|---|
| **Marekani** | **Simu: 1-757-365-3000** | **Email: law@smithfield.com** |
| **Poland** | **Simu: 22 2900033** | **Email: prawny@animex.pl** |
| **Romania** | **Simu: 0-800-800-053** | **arua pepe: office@smithfield.ro** |

3. Ikiwa mashaka yako yanahusisha ustawi wa wanyama au masuala ya kimazingira/utumishi wa aina iliyoelezwa kwenye **ukurasa wa 13**, unapaswa kuwasiliana na mratibu wa kimazingira wa sehemu yako ya biashara auor tSimu ya Moja kwa moja ya Smithfield kwenye **1-877-237-5270**.

4. Ikiwa una mashaka ya dharura au ikiwa ungependelea kuwasilisha mashaka yako bila kujulikana, piga simu kwa nambari ya Moja kwa Moja ya Maadili ya Smithfield kwenye**1-877-237-5270.** Simu kwenye simu ya moja kwa moja ni za siri na hata zinaweza kufanyika bila utambulisho, ingawa jinsi unavyotoa habari nyingi kwa mwendeshaji anayepokea simu, ndivyo tunavyoweza kushughulikia mashaka yako vyema zaidi. Ukiukaji wote ulioripotiwa wa Kanuni hii kupitia simu ya moja kwa moja huchunguzwa.

## Kumbusho:

Utalindwa kutokana na ulipizaji kisasi wa aina yoyote kwa kuwasilisha maswali au mashaka kwa yoyote yan rasilimali hizi. Vyovyote utakavyochagua kuwasilisha mashaka, Smithfield inakushukuru kwa kuwa tayari kufanya hivyo **SEMA!** Kwa usaidizi wako katika kuwasilisha mashaka mara moja, tunaweza kutimiza lengo letu za kukuza mazingira ya kimaadili ya biashara.

## Neno la Mwisho

Sote tuna wajibu sawa wa kutenda kimaadili na kwa kuzingatia kikamilifu Kanuni na sheria hii. Yeyote anayekosa kutimiza wajibu huo anaweza kutarajia kuadhibiwa. Adhabu kama hiyo inaweza kujumuisha ukomeshaji wa ajira.

Kanuni hii hutumika kwa Idara, vitengo na tanzu zote za kigeni au za eneo za Smithfield, na pia kwa ushirika na ubia ambapo Smithfield ina wajibu mkubwa wa maslahi na/au usimamizi.

Kanuni hii ya Mwendendo na Maadili ya biashara huweka matarajio rasmi ambayo hutumika kwa kila mfanyakazi bora ameajiriwa na Smithfield. Kwa kuongezea, baadhi ya sheria (ikijumuisha zile zinazolinda habari ya siri na ya umiliki ya kampuni) huendelea kutumika kwa watu wanaoacha kufanya kazi katika Smithfield, kwa hiari au pasipo hiari. Ilkiwa una maswali au mashaka kuhusu jinsi ya kuizingatia Kanuni hii au kuhusu mienendo ya watu wengine, unapaswa **KUSEMA!** kwa haraka.

Ikiwa sheria itagongana na sera au shughuli iliyowekwa na Kanuni, lazima utii sheria, lakini ikiwa utamaduni au sera ya eneo inagongana na Kanuni, Lazima uifuate Kanuni.